

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



TANZANIA YASAINI MAKUBALIANO YA MAENDELEO NA

UMOJA WA NCHI ZA ULAYA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini mkataba na Jumuiya ya nchi za Ulaya (EU) wa kiasi cha Euro 370 sawa na bilioni 749.5 za Kitanzania, kwa kipindi cha miaka sita ili kusaidia juhudi za kuleta maendeleo ya Tanzania katika sekta mbalimbali za umma. Hayo yamesemwa na Waziri wa Fedha na Uchumi Mhe. Mustafa Haidi Mkulo wakati wa kusaini mkataba huo.

Waziri alifafanua kuwa msaada huo uliotolewa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya ni wa kuchangia Bajeti ya Serikali na kusaidia sekta mbalimbali ili kutimiza malengo ya milenia ya mkakati ya kupunguza umaskini kwa wananchi.

Tanzania ni mojawapo kati ya nchi saba barani Afrika zitakazonufaika na msaada huo. Tanzania imepata kiasi kikubwa cha fedha ili iweze kutimiza malengo ya maendeleo ya milenia. Katika fedha hizo kiasi cha Euro milioni 5.0 zitapelekwa kusaidia Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Euro milioni 70.0 zitapelekwa upande wa miundombinu.

Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya umeongeza msaada nchini kutokana na Tanzania kuleta maendeleo katika maeneo mbalimbali kama vile barabara, sekta ya afya, utawala bora na kupiga vikali vita juu ya rushwa, alieleza Mh. Waziri.

Malengo ya milenia yaliyowekwa na nchi wahisani ili kusaidia nchi za Afrika yanatekelezeka hasa katika kupunguza umasikini kwa wananchi na kuleta

maendeleo katika sekta mbalimbali hayo yameelezwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi Bw. Ramadhani Khijjah.

Aidha Balozi anayewakilisha nchi za Umoja wa Ulaya Mhe. Tim Clarke alieleza kuwa serikali na wabia wa maendeleo, hivi karibuni wamemaliza mapitio ya mwaka wa maendeleo ya Tanzania. Hali ya mapitio hayo sio nzuri kwenye utekelezaji wa maendeleo katika sekta ya umma. Alitoa mfano kama vile utendaji wa hali ya chini wa bandari na reli, ambayo miundombinu yake imedorora, vilevile alieleza kuhusu suala la rushwa ambapo vyombo vya habari vinaandika sana maswala ya ufidadi na upotevu mkubwa wa fedha za umma, lakini alikiri kuwa Tanzania ina mwelekeo mzuri katika utendaji wake wa kazi na uletaji maendeleo katika sekta mbalimbali ndio maana Umoja wa Nchi za Ulaya umeiongezea Tanzania msaada ili kufanikisha maendeleo ya Tanzania.

IMETOLEWA NA MSEMAJI MKUU

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

14/12/2009